# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TATU

**29 JANUARI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 29 JANUARI, 2026

## I. DUA:

## II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

## III. MASWALI YA KAWAIDA:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**40. MHESHIMIWA IBRAHIM MOHAMED SHAYO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya inayojengwa Kata ya Ng'ambo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

**41. MHESHIMIWA PASCAL LUCAS LUTANDULA (CHATO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kukipandisha Kituo cha Afya Bwanga kuwa Hospitali ya Wilaya.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**42. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kila Mtoto anayezaliwa Halmashauri ya Mji Ifakara anapata Cheti cha kuzaliwa kwa wakati.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**43. MHESHIMIWA KAFITI WILLIAM KAFITI (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani kulipa fidia au kuruhusu Wananchi kuendeleza maeneo yao baada ya mgogoro wa muda mrefu na *Airport* - Mwanza.

**WIZARA YA UJENZI:**

**44. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Chalinze, Gwata, Magindu, Mpalu, Utete, Rufiji, Tumbi, Boko, Soga na Kongowe - Soga.

**WIZARA YA KILIMO:**

**45. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wananchi wa Kata ya Kihurio wanaotegemea Mto Saseni kwa umwagiliaji ambao kwa sasa umeharibika sana.

**46. MHESHIMIWA MORRIS JOSEPH MAKOI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya kutoa Pembejeo za Ruzuku kwa Wakulima wa Kahawa Moshi Vijijini.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**47. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza Mnada wa Mifugo wa Magena.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**48. MHESHIMIWA SAIDI SALIM HAMAD (OLE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Jimbo la Ole kwa kuwa halina Kituo cha Polisi.

**WIZARA YA AFYA:**

**49. MHESHIMIWA NAOMY DUNCAN MWAIPOPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kuhusu Homa ya Ini kwa Wananchi wa Kigoma.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa lijadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 14 Novemba, 2025.

***(Majadiliano Yanaendelea)***

**DODOMA**
**29 JANUARI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**